# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

## UKWELI KUHUSU CHANJO YA KUZUIA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI (HPV-VACCINE)

### UTANGULIZI

Saratani ya mlango wa kizazi ni mabadiliko ya ukuaji usio wa kawaida wa seli za mlango wa kizazi. Mabadiliko ya ukuaji wa seli hizi husababisha misuli au viungo vingine kuathirika mwilini.
Saratani hii inaweza kusambaa na kushambulia viungo vingine vikiwemo kibofu cha mkojo,uke na sehemu ya chini ya utumbo mkubwa na baadaye viungo kama figo, ini nk.
Saratani ya mlango wa kizazi ina athari kubwa kwa akina mama kote duniani. Inakadiriwa kuwa,duniani kote wastani wa wanawake 466,000 wanagundulika kuwa na Saratani ya mlango wa kizazi kila mwaka, wengi kati ya wanaoathirika wakitokea katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Saratani ya mlango wa kizazi ni ya pili miongoni mwa saratani zinazowaathiri wanawake nchini Tanzania ikiifuatia saratani ya matiti
Saratani ya mlango wa kizazi inaongoza kwa kusababisha vifo vya akina mama vinavyosababishwa na saratani.Inakadiriwa kuwa hapa Tanzania takribani wanawake 670 hupata saratani ya mlango wa kizani kila mwaka.

### NINI KINASABABISHA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI

Karibu saratani zote za mlango wa kizazi husababishwa na virusi vya Human Papilloma (HPV) ambavyo huambukizwa kwa njia mbalimbali ikiwemo kujamiiana.Vipo virusi vya HPV aina zaidi ya 40 vinavyoweza kusababisha maambukizi kwenye via vya uzazi vya wanaume, wanawake na vile vile mdomoni na kwenye koo. Aina ya 16 na 18 ya virusi vya HPV ndio husababisha asilimia 70 ya saratani zote za mlango wa kizazi duniani. Wanawake walio wengi wanaopatwa na virusi hivi hawapati saratani,bali asilimia 10 ndio hupata dalili za awali za saratani baada ya maambukizi ya muda mrefu na saratani yenyewe baada ya miaka kati ya 10 hadi 20.Human Papilloma Virus (HPV) ni aina ya virusi ambavyo vinaambukizwa kirahisi na inaaminika asilimia 70 ya watu duniani wameambukizwa na virusi hivi katika maisha yao..
Hii ina maana kuwa watu saba kati ya kumi walishapata virusi hivi katika maisha yao. Mara nyingi maambukizi ya HPV hayaoneshi dalili zozote na maambukizi yanaweza kutoweka bila kusababisha ugonjwa wowote. Lakini utafiti umeonesha kuwa asilimia 10 ya watu walioambukizwa hubaki na virusi hivi mwilini.

### SABABU ZINAZOCHANGIA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI

**Visababishi vya maambukizi ya HPV ni pamoja na:**

- Kuanza kujamiiana katika umri mdogo
- Kuwa na ndoa za mitala
- Uvutaji sigara
- Kuzaa watoto wengi
- Kuwa na wapenzi wengi

### DALILI ZA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI

**Hujitokeza ikiwa imeshasambaa na kuonesha dalili zifuatazo:-**

- Kutokwa damu ya hedhi bila mpangilio
- Kutokwa damu baada ya kujamiiana
- Maumivu ya mgongo, miguu na au kiuno
- Kuchoka, kupungua uzito, kupungukiwa au kokosa hamu ya kula
- Kutokwa uchafu wa rangi ya kahawia au wenye damu kwenye uke
- Maumivu ya miguu au kuvimba

**Dalili mbaya zaidi zinazoweza kujitokeza ni pamoja na kuishiwa damu, figo kushindwa kufanya kazi, kupatwa na fistula, na uvimbe wa tezi.**

### JINSI YA KUKINGA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI

**Shirika la Afya duniani linapendekeza hatua tatu za kufuata katika kukinga saratani ya mlango wa kizazi:**

- Kupata chanjo ya HPV, kutokufanya ngono katika umri mdogo, kuepuka kubeba mimba katika umri mdogo, kuwa na mwenzi mmoja mwaminifu ,kutumia kondomu na kuepuka uvutaji wa sigara.
- Kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini dalili za awali na kupata matibabu stahiki mapema.
- Matibabu maalum kwa mtu ambaye tayari amepata saratani ya mlango wa kizazi

**Utambuzi wa saratani ya mlango wa kizazi unatakiwa kufanywa na Wataalamu wa afya na endapo itagundulika mapema inaweza kutibiwa.**

### CHANJO YA KUZUIA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI (HPV - VACCINE)

Chanjo ya HPV ni kinga dhidi ya virusi vya HPV; ni salama na imethibitishwa na kuidhinishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA). Chanjo hii hutolewa kwa wasichana wenye umri wa kati ya miaka 9 hadi 14. Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa chanjo hii inaleta matokeo chanya pale inapotolewa katika umri huu na hutoa kinga ya muda mrefu. Hapa nchini Tanzania, chanjo hii itatolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya na huduma za mkoba hususani shuleni na kwenye jamii katika utaratibu wa kawaida wa utoaji wa huduma za chanjo.

### WALENGWA NA RATIBA YA CHANJO YA HPV

Chanjo hii inatolewa katika dozi mbili (2) ili kupata kinga kamili dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi.
Nchini Tanzania dozi ya kwanza ya chanjo hii itatolewa mara walengwa wafikishapo umri tajwa hapo chini ikifuatiwa na dozi ya pili miezi sita (6) baada ya dozi ya kwanza kwa utaratibu ufuatao:

**1. Mwaka 2018 ni wasichana wote wanao timiza umri wa miaka kumi na nne (14)**

Walengwa wote wataandikishwa kwenye rejesta na watakaopata chanjo watapatiwa kadi maalum inayothibitisha kuwa wamepata chanjo. Kadi hii itaonesha pia tarehe ya kurudi kwa ajili ya dozi ya pili na tarehe ambayo mlengwa amekamilisha ratiba yake ya chanjo kwa kupata dozi ya pili.



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

## UKWELI KUHUSU CHANJO YA KUZUIA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI (HPV-VACCINE)

## UJUMBE MUHIMU KWA JAMII

- Chanjo ya HPV inawakinga wasichana dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi pindi waipatapo katika muda stahiki
- Wanawake walio na umri kati ya miaka 30 na 50 wajitokeze katika vituo vya afya kote nchini ili kufanyiwa uchunguzi mara kwa mara ili kubaini mabadiliko ya awali katika via vya uzazi.
- Chanjo ya HPV ni salama na imethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA).
- Wasichana wote wanatakiwa kupata dozi mbili za chanjo ya HPV ili waweze kupata kinga kamili.
- Chanjo hii inatolewa bila malipo katika vituo vya kutolea huduma za afya, wakati wa huduma za mkoba na shuleni.

## UJUMBE MAHUSUSI

- Chanjo ya HPV inawakinga mabinti dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi hapo baadae watakapokuwa katika familia zao.
- Saratani ya mlango wa kizazi huathiri via vya uzazi vya wanawake na inaongoza kwa vifo miongoni mwa wanawake walio katika umri wa kubeba ujauzito
- Mabinti wanapaswa kupata chanjo ya HPV wakiwa katika umri mdogo.
- Unaweza kumlinda binti yako na maisha yake ya baadae kwa kumpatia chanjo
- Chanjo ni salama ,haina madhara na haimzuii binti yako kutopata watoto katika maisha yake ya baadae.
- Chanjo ya HPV inapatikana wakati wowote,bila malipo katika vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali na watu binafsi.
- Chanjo hii inatolewa dozi mbili,dozi ya pili hutolewa miezi sita baada ya dozi ya kwanza

. Ni muhimu kukamilisha dozi mbili ili kupata kinga kamili


**IMETAYARISHWA NA:**
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO,**
**CHUO KIKUU CHA DODOMA,**
**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI YA MAENDELEO YA JAMII,**
**JENGO NA: 11,**
**S. L. P. 743,**
**40478 DODOMA.**
**SIMU: +255 026 2323267 | TOVUTI: www.moh.go.tz**